**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**April, 2024**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**


**Namba ya usajili (NECTA) : S 1578**

**Mkuu wa Shule: 0757037153**

**Makamu Mkuu wa Shule: 0754012648/0620416520**
**Matron/Patron: 0758217799/0754241254**

**Shule ya Sekondari CHANGARAWE**

**S.L.P.126, MAFINGA**


**Tarehe ………………………………**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**……………………………………………**

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI CHANGARAWE HALMASHAURI YA MJI MAFINGA MKOA IRINGA MWAKA 2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024 na atasoma tahasusi ya ………….

Shule ya Sekondari Changarawe ipo umbali wa Kilometa 4 kutoka stendi kuu ya mabasi ya Mji wa Mafinga. Usafiri wa kufika shuleni unapatikana katika kituo cha mabasi Mafinga Mjini. Nauli ni Shilingi 2000/= kwa pikipiki na Shilingi 3000/= kwa bajaji na Shilingi 5000/= kwa taksi.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe ………………………… hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe …………………. .

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

**SARE ZA SHULE - WAVULANA**

- Suruali mbili (02) kitambaa AMERICAN KHAKI zilizoshonwa kwa heshima iwe na mkunjo chini (turnerup). Marufuku mshono wa JEANS AU MLEGEZO, AU suruali inayobana (kitambaa kimeambatanishwa).
- Mashati mawili meupe ya mikono mirefu yasiyo angaza.
- Koti American Khaki lililoshonwa kwa Heshima ili kufanya suti lisiwe na mipasuo nyuma. (Tunashauri ushonewe sare za shule kwa mafundi wa hapa Mafinga kuepuka kuchanganya rangi / Kitambaa).
- Tai iliyoshonwa kwa Heshima ya kitambaa cheusi bila maua
- Viatu vya ngozi jozi mbili (02) rangi nyeusi vya kamba, Boots na viatu vya kuchomekea haviruhusiwi kabisa.
- Soksi jozi mbili (02) rangi nyeusi.
- Mkanda wa suruali – rangi nyeusi (usio na urembo)
- Nguo za kushindia (shamba dress) suruali mbili (2) za dark blue mshono sawa na sare ya shule na t-shirt mbili za rangi ya Maroon / Damu ya mzee zisizo na maua (zenye kola au form six)
- Pulneck nyeusi na nyeupe na Jacketi zito jeusi
- Truck suit rangi ya Dark bluu pea moja.
- Jezi ya michezo rangi ya bluu (bukta na tishirt)
- Raba za michezo / viatu vya michezo

**NB: Nguo zingine haziruhusiwi.**

**WASICHANA**

1. Sketi za rangi ya American Khaki mbili rinda boksi ndefu kufika chini iguse visigino, makoti mawili (ya kitambaa cha sketi) ili kufanya suti yasiyo na mipasuo nyuma (Kitambaa kimeambatanishwa). Pia tunashauri ushonewe kwa mafundi wa hapa Mafinga kuepuka kuchanganya rangi na kitambaa.
2. Rangi ya hijab(kijuba) iwe nyeupe isiyo na urembo kwa wanafunzi wa kiislamu
3. Mashati meupe mikono mirefu mawili (2) pamoja na tai nyeusi bila maua
4. Soksi nyeupe ndefu jozi mbili.
5. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi visiwe simpo na kufunga na Kamba.
6. Truck suit rangi ya Dark bluu na mwanafunzi wa Kiislamu anaruhusiwa kuja na short kanzu nyeupe.
7. Nguo za kushindia (shamba dress) sketimbili (2) dark blue mshono kama wa sare za shule na T-shirt 02 rangi ya Maroon /Damu ya mzee (zenye kola au form six)
8. Jezi ya michezo rangi ya bluu (bukta na tishirt).
9. Pulneck nyeusi na nyeupe na Jaketi zito jeusi
10. Raba za michezo / viatu vya michezo.

**NB: Nguo nyingine haziruhusiwi kabisa.**

### 2.1 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i) Ream ya karatasi 01 (A4 photocopy paper)Kwa kila muhula

ii) Godoro la futi 2 ½ kwa futi 6.
iii) Mashuka pea 2 rangi ya pink, blanketi 1 nzito, mto 1 Na foronya 2 rangi ya pinki
iv) Vyombo vya chakula (sahani, bakuli (au containa), kijiko na kikombe)
v) Ndoo 2 zenye mfuniko, ujazo wa lita kumi (10)
vi) **MCHEPUO WA HGK**: Jembe 1 lenye mpini imara, Fagio ya chelewa 1, fagio 01 squizer na fagio laini ya ndani.
vii) **MCHEPUO WA HGL**: jembe1 lenye mpini imara, fagio ya chelewa 1 na fagio 01 Ngumu (brush)na fagio squizer 1
viii) **MCHEPUO WA HKL: Mopa 1 na ndoo yake pamoja na Reki 01 yenye mpini**
ix) Kanda mbili jozi moja
x) Kila mzazi/mlezi unaombwa kumpa fedha ya matumizi yake binafsi ikiwemo nauli ya kwenda na kurudi nyumbani wakati wa likizo.
xi) Aje na nakala (coppy) ya result slip ya O-level
xii) Aje na Nakala (coppy) ya cheti cha kuzaliwa.
xiii) Viatu vya wazi (Sandles) za kufunga au simple shoose
xiv) Tranka 01
xv) Mafuta ya kupaka, dawa meno, mswaki, sabuni nk (MANUKATO KAMA PAFYUMU NA CREAM HAZIRUHUSIWI).
xvi) Taulo .
xvii) Kanga/ kitenge kwa wasichana.

**NB: TUNASHAURI MZAZI /MLEZI AMKATIE BIMA YA AFYA MWANAFUNZI**

**a) MAHITAJI YA TAALUMA**

i) **Daftari counter book 7 na daftari ndogo 7**
ii) **Peni, pencil, ruler na mkebe. nk.**
iii) **Vitabu vya masomo ya Tahasusi husika.**

**ANGALIZO**: Mwanafunzi alete kifaa kulingana na tahasusi anayosoma.

## 2.1 Michango mbalimbali

### a) Shule za Bweni

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Fedha hii Ikalipwe kwenye akaunti ya shule 60201200061 NMB Bank Changarawe Sekondari**

## 3.Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).**

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**3.3 Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

4.Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

……………………………………

**PETER J MBATA**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule : 0757037153**
- **Makamu Mkuu wa Shule : 0620416520**
- **Mwandamizi Taaluma : 0755310695**
- **Mwandamizi Malezi: 0754241254**

## 1. FOMU YA MAELEZO BINAFSI KUHUSU HISTORIA YA MWANFUNZI /MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI

......................................

....................................

....................................

MKUU WA SHULE,

SHULE YA SEKONDARI CHANGARAWE,

S.L.P. 126.

**MAFINGA**

**YAH: KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI CHANGARAWE ILIYOKO MAFINGA- MKOA WA IRINGA**

Mimi mwanafunzi............................................... Kidato cha .................. Mwaka....................

1. Nilizaliwa mnamo mwaka (Taja tarehe, mwezi na mwaka)...................... kijiji/Mjini....................

Nimesoma shule ya sekondari ya ..................................... Wilaya ya..............Mkoa wa ....................

- Nilikuwa kiongozi wa ...................................................................
- Sikuwa kiongozi.............................................................
- Michezo niipendayo ni .......................................................................
- Nina kipaji cha........................................................
- Mengineyo Niwezayo..........................................................

2. Naahidi kuwa mtiifu wa sheria za shule, kutoshiriki katika mgomo, fujo, makosa ya jinai, dharau kwa walimu, dharau kwa viongozi wa ngazi zote au wowote wale.

Nitakuwa na nidhamu ya kujituma, kusoma kwa bidii na kwa mfano bora kwa wanafunzi wengine.

Tofauti na haya niondolewe shuleni mara moja.

Jina la mwanafunzi………………………………….. sahihi……………… kidato…………………... tarehe ……………

**2. FOMU YA MZAZI/MLEZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA , KANUNI NA MAELEKEZO MENGINE HALALI YATAKAYOTOLEWA NA SHULE**

……………………………………………

…………………………………………..

……………………………………………..

MKUU WA SHULE,

SHULE YA SEKONDARI CHANGARAWE,

S.L.P. 126,

**MAFINGA**

**YAH: KUKUBALI KUJIUNGA MWANANGU NA SHULE YA SEKONDARI CHANGARAWE ILIYOKO MAFINGA-MKOA WA IRINGA**

MWANAFUNZI ……………………………………………………………………

KIDATO CHA TANO MWAKA 2024

1. Mimi …………………………………………………………….

Mzazi /mlezi wa mwanafunzi aliyetajwa hapo juu. Nakiri kuwa nimeelewa maelekezo yote yaliyotolewa na masharti ya fomu hii.

2. Nakubali mwanangu aendelee na masomo na nitatekeleza yale yote yanayonihusu kwa wakati wake. Kama ilivyoagizwa katika maelekezo ya kujiunga na shule.
3. Naahidi kumhudumia mtoto wangu kwa hali na mali ili kufikia malengo yake ya kujiunga na shule hii.
4. Naahidi kusimamia nidhamu na maendeleo yake muda wote awapo hapa shuleni.
5. JINA LA MZAZI / MLEZI ………………………………………………… SAHIHI……………………….
6. ANWANI YA MZAZI/MLEZI……………………………………….
7. NAMBA YA SIMU …………………………………… TAREHE ……………………………

**FOMU YA KUPIMA AFYA YA MWANAFUNZI**

**03. (FOMU YA KUPIMA AFYA YA MWANAFUNZI)**

**SEHEMU A**

SHULE YA SEKONDARI CHANGARAWE,

S.L.P. 126,

**MAFINGA**

**…………………………..**

***KUMB.NA.MTC/CHSS/JI/2024/F5/10***

MGANGA MKUU,

HOSPITALI YA SERIKALI YA

………………………………………………..

S.L.P…………………..

**MAFINGA**

**YAH: FOMU YA KUPIMWA AFYA YA MWANAFUNZI**

Somo la hapo juu lahusika.

Tafadhari tunaomba umpime mwanafunzi aliyetajwa hapo juu wa kidato cha TANO mwaka 2024; kwa gharama za mzazi/mlezi wake.

Ni muhimu apimwe ili kujua afya yake kabla ya kuripoti hapa shuleni na kuendelea na masomo.

**Natanguliza shukrani**

**……………………………………**

**PETER JOHN MBATA**

**MKUU WA SHULE**

3. **<u>FOMU HII IJAZWE NA MGANGA MKUU WA MKOA /WILAYA NA MWANAFUNZI AJE NAYO SHULENI NA KUIKABIDHI KWA MKUU WA SHULE.</u>**

**SEHEMU B**

Mimi (Jina la Mganga Mkuu wa Mkoa/Wilaya) ……………………………………………..

Ninathibitisha kuwa mwanafunzi huyu (Jina la mwanafunzi)…………………………………..

Amepimwa na mimi kikamilifu na kuonekana kuwa anayo /hana afya nzuri kwa mujibu wa taarifa zifuatazo;

**(A) <u>Hali ya Mwili</u>.**

(i) Mapigo ya moyo…………………………………………………………
(ii) Damu (Haemoglobin)………………………………………………..…..
(iii) Kundi la Damu (Blood group)……………………….……………………...
(iv) Mkojo…………………………………………………………………
(v) Haja kubwa…………………………………………………………………
(vi) Macho …………………………………………………………………….
(vii) Masikio ……………..…………………………………………………..

NB. Weka maoni yako kuhusu kile kilichotajwa…………………………………..

…………………………………………………………………………………….

…………………………………………………………………………………….

**(B) <u>Magonjwa.</u>**

Amewahi /hajawahi au hana magonjwa yafuatayo;

(a) Kifua kikuu (TB)……………………………………………………….…
(b) Kifafa (Epilepsy)…………………………………………………………
(c) Shinikizo la damu (BP)…………………………………………………..
(d) Magonjwa ya tumbo ……………………………………………………..
(e) Seli mundu (Sickle cells)…………………………………………….……
(f) Ukoma……………………………………………………………………
(g) Magonjwa ya zinaa (taja aina)……………………………………………
(h) Ugonjwa wa akili ……………………………………………………..…
(i) Ugonjwa mwingine nje ya orodha hapo juu ………………………………..

……………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………..

**Maoni ya Daktari** ……………………….…………………………………………………

………………………………………………………………………………

Saini na Muhuri wa Daktari/ Mganga wa Hospitali ya Serikali